JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

S.L.P 1951,

Simu: 027-2750885;

Nukushi:027- 2750889

Barua pepe: rbckilimanjaro@pccb.go.tz

Wavuti: www.pccb.go.tz

KILIMANJARO – JULAI 2022

TAKUKURU KILIMANJARO WAFUATILIA MIRADI YA MAENDELEO YA SH. BILIONI 7.1

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Kilimanjaro imeendelea na utekelezaji wa majukumu yake katika robo ya mwisho ya mwaka ya kuanzia Aprili - Juni, 2022 ambapo mkazo uliwekwa katika kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo imeletwa kwa wingi katika mikoa na tulilenga kuhamasisha wananchi ili washiriki kikamilifu katika kuhakikisha miradi hiyo inakamilika kwa viwango bora, kwa wakati na kama ilivyokusudiwa ili iweze kuwanufaisha. Katika kipindi husika, TAKUKURU Mkoa wa Kilimanjaro;-

MOSI

Imefuatilia utekelezaji wa miradi yenye thamani ya Jumla ya shilingi **bilioni saba nukta moja** (7,133,130,274.6/=)

Kazi zilifanyika katika kufuatilia fedha za miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

	MRADI	**THAMANI**
1.	Mradi wa ujenzi wa madarasa- Rasesa shule ya sekondari	Tsh. 40,000,000/-

2	Mradi wa ujenzi wa madarasa- Himo shule ya sekondari	Tsh. 40,000,000/-
3.	Ujenzi wa kituo cha afya, mradi wa maji na ujenzi wa madarasa- Miwaleni	Tsh. 3,155,561,732/-
4.	Mradi wa maji ya bomba –Manda chini- Rombo	Tsh. 248,980,500/-
5.	Ujenzi wa vyumba 8 vya madarasa shule ya sekondari Mamsera- Rombo	Tsh. 154,505,952/-
6.	Mradi wa maji –Kivisini-kwanyangewenye- Mwanga	Tsh. 433,414,948/-
7.	Ujenzi wa Barabara ya CD Msuya –Kiruru Mwanga	Tsh. 668,283,642.60/-
8.	Mradi wa maji unaotekelezwa na RUWASA Rundugai - Kawaya- Hai	Tsh. 558,982,655/-.
9	Ujenzi wa mradi wa maji Kisiwani unaotekelezwa na Ruwasa-Same	Tsh. 500,000,000/-
10	Mradi ya ujenzi wa kituo cha afya Ruvu- Same	Tsh. 259,959,000/-
11	Ukarabati wa zahanati ya mtii- Same	Tsh. 50,000,000/-
12	Ujenzi wa vyumba vine vya madarasa ya shule ya sekondari kwambegu- Same	Tsh. 70,424,500/-
13	Ujenzi wa kituo cha afya kata ya Oklili- Siha	Tsh. 250,000,000/=
14	Ujenzi wa shule ya sekondari kata ya Biriri- Siha	Tsh. 470,000,000/=
15	Ujenzi wa Barabara ya lami DC Karasi-Siha	Tsh. 535,000,000/-
16	Ujenzi wa nyumba (three in one) ya Zahanati ya kijiji cha Roseline Siha	Tsh. 90,000,000/=
17	Ujenzi wa wodi ya wanawake Hospitali ya Wilaya ya Siha	Tsh. 167,000,000/=

Katika kufuatilia fedha za utekelezaji wa miradi hiyo, mapungufu kadhaa yalibainika zikiwemo kasoro za kiufundi yaani mapungufu ya vipimo mbalimbali kama fremu za milango na madirisha na pia ubora wa milango kuwa tofauti na uliopaswa kuwepo.

Tunawakumbusha na kuwahimiza wote wenye wajibu wa kufanyia kazi maazimio ya kuziba mianya ya rushwa bainishwa, kutelekeza wajibu wao kwa wakati.

PILI

Katika hatua nyingine,TAKUKURU mkoa wa Kilimanjaro katika kuhamasisha wananchi kushiriki katika kusimamia miradi hiyo mingi ya maendeleo ilitoa elimu dhidi ya rushwa kupitia semina 10, Makala 10, maonesho 8 vipindi vya redio 9, Uimarishaji wa klabu za wapinga rushwa 116 na mikutano ya hadhara 15.

TATU

Pamoja na kuhamasisha sana suala zima la **KUZUIA RUSHWA,** bado wapo wachache ambao ni wamekuwa ni kama sikio la kufa, lisilosikia dawa na wameendelea kujihusisha na vitendo vya rushwa na ubadhirifu.

Katika kipindi husika, tulipokea taarifa za **malalamiko 97**, ambapo taarifa zilizohusu rushwa zilikuwa 61 na zisizo za rushwa ni 36.

- Taarifa zinazohusu rushwa zilihusu sekta au maeneo yafuatayo: Serikali za mitaa 18, Elimu 15, Afya 9, Polisi 15, Mahakama 7, Ardhi 11 na sekta binafsi kila mmoja 10 na sekta nyinginezo 12.

- Taarifa zilizohusu rushwa zimeshughulikiwa kwa mujibu wa sheria kwa njia za uelimishaji taarifa 12, hizi ni taarifa zilizohusu miradi ambapo wahusika kwa mfano Kamati za Ujenzi walibainika kutokuwa na ufahamu wa nini hasa wanatakiwa kufanya katika ujenzi na pia wananchi walielekezwa wajibu wao wa kushiriki katika kusimamia na kuilinda miradi husika kwa kuwa wao wanaishi maeneo ya miradi hiyo na kwamba miradi hiyo inawanufaisha wao moja kwa moja.
  - Taarifa 10 zilifanyiwa kazi kwa njia ya uzuiaji yaani ukaguzi wa miradi na kushauri marekebisho kwa gharama za mafundi. Vilevile, ilishauriwa kuwa taarifa za mapato na matumizi ya vijiji zisimamiwe ili zisomwe kwa wananchi.
  - Pia uchunguzi wa Majalada 12 ya uchunguzi yamekamilika na majalada 27 yanaendelea na uchunguzi.

TAKUKURU Mkoa wa Kilimanjaro, kwa kushirikiana na wasimamizi na wadau wengine wa maendeleo, waliwataka wakandarasi wa miradi hiyo kurekebisha kasoro zilizobainika na kuhakikisha thamani ya fedha inapatikana katika miradi hiyo.

Katika hatua nyingine, pale ambapo eneo la utendaji au utoaji huduma linaonekana kulalamikiwa sana kuwa na viashiria vya rushwa, TAKUKURU hufanya **uchambuzi wa mfumo** ili kubaini iwapo kuna mianya ya rushwa na hatimaye kushauri namna bora ya kuiziba mianya hiyo. Hivyo, katika kipindi husika, kwa lengo la kudhibiti vitendo vya rushwa, TAKUKURU Mkoa wa Kilimanjaro ulifanya chambuzi za mifumo katika maeneo nane (8) yafuatayo:-

S/No	CHAMBUZI-IDARA	KITUO/WILAYA
1	Wakala wa Ufundi na Umeme - TEMESA	Same
2	Usimamizi wa Mitihani ya Taifa unaofanywa na Askari Mgambo	Mwanga
3	Uendeshaji wa Mabaraza ya Kata	Hai
4	Mfumo wa sheria ndogo za mazingira - Kata ya bondeni na mawenzi	Moshi manispaa
5	Mfumo wa tozo za mazao ya madini	Halmashauri ya Moshi
6	Mfumo wa matibabu ya wazee	Halmashauri ya Moshi
7	Mfumo wa utoaji wa vibali katika uchimbaji madini ya ujenzi	Siha
8	Mfumo wa matumizi ya Mashine za POS	Siha

- **Warsha tano** za kujadili matokeo ya chambuzi za mifumo kwa kushirikisha wadau zilifanyika katika sekta ya usimamizi wa misitu, ambapo maazimio ya namna ya kuziba mianya ya rushwa yalifikiwa na muda wa utekelezaji kuwekwa. Vile vile, ufuatiliaji wa utekelezaji wa maazimio yaliyofikiwa siku za nyuma katika sekta za ardhi na afya ulifanyika na kubaini kuwa maazimio yanatekelezwa.

- Taaarifa 36 zisizohusu rushwa, 5 zilihamishiwa Idara nyingine na wahusika wa taarifa 31 zilizosalia walishauriwa mahali sahihi pa kuziwasilisha kwa msaada na hatua zaidi hivyo taarifa hizo zikafungwa.

- Katika kipindi husika, Mashauri 16 mapya yamefunguliwa mahakamani na kufanya jumla ya mashauri yanayoendelea mahakamani kufikia 36.
    - Idadi ya mashauri yaliyoamuliwa katika kipindi hicho ni 04, ambapo kati ya hayo, Jamhuri ilishinda mashauri matatu (03) na kushindwa moja (01).

- Tunaendelea kuwasihi wananchi wa mkoa wa Kilimanjaro, kufuatilia elimu tunazotoa ili watuletee malalamiko yanayoangukia kwenye Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa sura ya 329 kwani bado wengi wanawasilisha kwetu masuala yanayohusu mamlaka nyingine.

NNE

MIKAKATI YA Julai – Septemba, 2022

TAKUKURU Mkoa wa Kilimanjaro, katika robo ya kwanza yaani Julai – Septemba 2022, tunatarajia kuimarisha na kuongeza juhudi za uzuiaji rushwa kwa kuongeza idadi ya wananchi watakao elimishwa ili kuongeza ushiriki wao katika mapambano dhidi ya rushwa na pia kuongeza ufuatiliaji wa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika mkoa wetu ili kupata thamani ya fedha katika kila mradi.

Pia tutaendelea kufuatilia makusanyo na uwasilishaji wa mapato yanayotokana na mashine za POS na kuchukua hatua stahiki kwa wale watakaobainika kufuja mali za umma.

Aidha, tutafanya warsha na wadau kujadili matokeo ya chambuzi za mifumo zilizokamilika ili kuweka maazimio ya namna bora ya kuiziba mianya ya ufujaji iliyobainishwa.

Mwisho, Tunawashukuru wanahabari wote walioshiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya rushwa kwa kuhabarisha umma juu ya vita dhidi ya rushwa na tunawashukuru wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro kwa

kutuunga mkono katika vita hii. Vita hii ni yetu sote hivyo tunawasihi wengine wote wenye mtazamo kwamba hii ni kazi ya Serikali pekee, waachane na fikra hizo batili na waungane nasi kuongeza nguvu katika Jeshi la Wazalendo, Waadilifu na wanaojisikia fahari kuzuia rushwa.

SENSA KWA MAENDELEO YA TAIFA JIANDAE KUHESABIWA

ZUIA, ELIMISHA, PAMBANA, TOKOMEZA RUSHWA - inawezekana.

Iimetolewa na,

Frida S. Wikesi
Mkuu wa TAKUKURU (M)
Kilimanjaro

Simu: 0738150110